




**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



**AIDS Free**  
Strengthening High Impact Interventions  
for an AIDS-free Generation

# Tohara ya Mwanaume

1

## KITENDEA KAZI CHA WAHAMASISHAJI JAMII JINSI YA KUFANYA KIKAO NA VIONGOZI WA KATA



### UTANGULIZI

Kitendea kazi hiki ni mwongozo kwa wahamasishaji jamii wa huduma ya tohara ya mwanaume. Ni kimojawapo katika kifurushi cha vitendea kazi kuhusu mada tofauti. Lengo lake ni kumwezesha mhamasishaji kuzingatia mambo na hatua muhimu kabla, wakati na baada ya kufanya kikao na wadau mahususi. Mhamasishaji anatakiwa kuelewa na kurejea maelekezo yaliyomo ili kuendesha kikao vizuri na kupata mafanikio makubwa.



### WAHUSIKA

Viongozi walioteuliwa au kuchaguliwa kisheria na kupewa mamlaka ya kusimamia shughuli za maendeleo katika jamii zao, mfano madiwani, mabalozi wa nyumba kumi, watendaji, wenyeviti na wajumbe wa serikali za mitaa.



### SIFA ZA WAHUSIKA

- Wana nguvu ya dola au siasa.
- Wanaheshimika kama wawakilishi wa jamii.
- Wanafahamu fika wakazi katika maeneo yao.
- Wapo katika ngazi zote za jamii.



### SABABU ZA KUWAHUSISHA

- Wana mamlaka ya kuruhusu au kukataza vikao kufanyika katika eneo lao.
- Wana taarifa muhimu kuhusu matumizi ya huduma ya tohara katika eneo lao.
- Wanaelewa vizuri jamii na kuweza kubainisha vitu vinavyoweza kuathiri huduma.
- Wanawajibika katika kutekeleza mikakati ya kitaifa na sera za serekali.

## HATUA MUHIMU KATIKA KUFANIKISHA KIKAO

1




### KABLA YA TUKIO

- **Tambua viongozi** unaohitaji kuwashirikisha kwenye kikao katika eneo lako.
- **Omiba idhini** kutoka kwa mamlaka ya halmashauri inayosimamia washiriki.
- **Shauriana na viongozi wako** kuhusu tarehe, idadi ya washiriki na mahitaji ya kikao.
- **Omiba mwakilishi** wa uongozi ambaye utashirikiana naye katika maandalizi.
- **Mjengee mwakilishi** ufahamu juu ya tohara na majukumu yake kwenye kikao.
- **Andao mada** kwa kushauriana na mwakilishi wa uongozi na viongozi wako.
- **Andao nyezo** za kikao mfano rejea, vitendea kazi, vipeperushi na mabango.
- **Omiba mamlaka** husika ya washiriki kutuma mwaliko kutumia taratibu zao.



# 2



# 3



## WAKATI WA TUKIO

- **Vaa uhusika** ikiwemo matumizi ya lugha sahihi na mavazi yanayoonyesha heshima.
- **Mwandaе mwakilishi** wa uongozi kukutambulisha na kutoa utangulizi kuhusu kikao.
- **Wasilisha mada** kwa kusitiza taarifa muhimu kama faida na athari ndogo ndogo za tohara, mahali na muda wa huduma, umri wa walengwa na gharama ya huduma.
- **Ruhusu muda wa majadiliano**, maswali na maazimio kwa kuwashirikisha viongozi na mwakilishi kutoa ufanuzi inapohitajika. Jibu mitazamo potofu ikijitokeza.
- **Toa shukrani** kwa mamlaka husika, mwakilishi wa uongozi na viongozi walioshiriki na watajje namba yako ya simu iwapo watahitaji kufanya mawasiliano baadaye.
- **Kamilisha taratibu za kiofisi** kama kujaza fomu ya mahudhurio na wajulishe washiriki kuwa utasubiri iwapo kuna mshiriki anataka kuwa na maongezi binafsi na wewe.

## NI MUHIMU

- Kuomba idhini ili kupata fursa ya kuyafikia makundi mbalimbali ndani ya jamii.
- Kutambua mazingira na mahitaji ya wahusika ili kupunguza au kuondoa changamoto.
- Kuwa makini katika matumizi ya lugha na kuheshimu miiko ya kundi husika.
- Kutoa shukrani kwa viongozi, wawakilishi na washiriki wote katika vikao.
- Kushauriana na viongozi wako katika hatua zote kwa taarifa na msaada unapohitajika.

## BAADA YA TUKIO

- **Wasilisha muhtasari wa kikao** kwa mamlaka iliyoidhinisha kikao na viongozi wako kwa taarifa na msaada katika kufanya kazi maoni, maazimio na changamoto.
- **Fuatilia maazimio ya kikao** kupitia mamlaka husika, ofisi za washiriki, simu za mkononi na kukutana ana kwa ana wa wahusika.
- **Jenga ukaribu** na viongozi rafiki na mwakilishi kuhakikisha mwendelezo wa ushirikiano.
- **Tumia majukwaa ya viongozi** mfano mikutano ya kijiji, kamati za maendeleo, kamati za UKIMWI na sherehe/maadhisho ya kitaifa kuhimiza viongozi kuunga mkono huduma ya tohara.

## ANGALIZO

Uwe mwangalifu katika kuchagua viongozi wa kata ambao utashirikiana nao. Hususan kuhusu itikadi zao za kisiasa na kidini. Hakikisha mchanganyiko wa wawakilishi bila kuegemea upande wowote ama kutilia mkazo itikadi yoyote. Hii itaepusha kuchochea mitazamo potofu juu ya huduma. Shauriana na mamlaka husika na viongozi wako.

## VYANZO VINGINE VYA KUJENGA UZOEFU KATIKA MADA

- Machapisho ya uhamashajii wa huduma ya tohara.
- Ufanuzi wa utekelezaji kutoka kwa viongozi wako.
- Ushauri wa kitaalamu kutoka kwa watoa huduma ya tohara.
- Taarifa za serikali kuhusu tohara, UKIMWI na saratani.

